

MRADI WA VIWANJA ELFU TANO KUWANUFAISHA WANANCHI WA MANISPAA YA BUKOBA

Halmashauri ya Manispaa ya Bukoba kwa kushirikiana na Taasisi ya uwekezaji Tanzania (UTT-AMIS) inaendelea na utekelezaji wa ubia wa mradi wa viwanja elfu tano(5,000)

Mkurugenzi wa Manispaa ya Bukoba Ndugu Hamadi A. Njovu amewataka wananchi kuendelea kununua fomu,kuonyeshwa viwanja na kununua viwanja.

Amesema hadi sasa jumla ya fomu zilizoununuliwa na kuwasilishwa ofisini ni fomu hamsini tu amewataka wananchi kuendelea kujitokeza na kuchagua viwanja.

Aidha Mkurugenzi huyo amesema ataendelea kutoa matangazo ya kuuza viwanja kupitia simu,(U-tube Kasibante Media na magrupu mbalimbali ya Whatsap, Redio na mbao za matangazo katika maeneo yenye mkusanyiko mkubwa.

Amesema bei ya viwanja imeshuka hadi elfu mbili kwa kila mita ya mraba ambapo bei hiyo ilipitishwa na Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Manispaa ya Bukoba

Aidha amewataka ambao hawakukamilisha malipo wanakumbushwa kukamilisha malipo hayo,Ameendelea kusema kuwa wananchi na taasisi walioongezea malipo baada ya kulipa fedha ya dhamana shilingi laki mbili lakini hawajakamilisha malipo ya kiwanja wakamilishe malipo hayo.